

Simu: +255-26- 2323201-7  
Nukushi: +255-26-2323208  
Barua pepe: [nje@nje.go.tz](mailto:nje@nje.go.tz)  
Tovuti: [www.foreign.go.tz](http://www.foreign.go.tz)



Mji wa Serikali,  
Mtumba,  
S.L.P 2933,  
40466 DODOMA

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### UAMUZI WA SERIKALI YA DENMARK KUFUNGA UBALOZI WAKE WA TANZANIA IFIKAPO MWAKA 2024

28 Agosti 2021, Washington, D.C.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeeleza kusikitishwa na hatua ya Serikali ya Denmark ya kuamua kufunga shughuli za Ubalozi wake nchini Tanzania ifikapo mwaka 2024.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula (Mb.) ameeleza masikitiko ya Serikali kufuatia hatua hiyo ya Denmark hasa ikizingatiwa jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita za kufufua na kuimarisha diplomasia na uhusiano na nchi rafiki ikiwemo Denmark, kuimarisha mazingira ya blashara na uwekezaji nchini pamoja na kuimarisha demokrasia na utawala wa sheria.

Waziri Mulamula ameyasema hayo jijini Washington, D.C. nchini Marekani tarehe 27 Agosti 2021 wakati wa mazungumzo kwa njia ya mtandao (Video Conference) na Mhe. Flemming Moller Mortensen, Waziri wa Ushirikiano wa Maendeleo wa Denmark kufuatia ombi la Waziri huyo kuzungumza na Waziri Mulamula. Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula yupo nchini Marekani kwa ziara ya klikazi.

Kwenye mazungumzo hayo, Waziri Mulamula amemueleza Waziri Mortensen kwamba, pamoja na hatua hiyo iliyochukuliwa na Denmark, ni matarajio ya Tanzania kuwa Serikali ya Denmark itaendelea kushirikiana na Tanzania kwenye masuala mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuunga mkono ajenda za Tanzania katika Umoja wa Ulaya, Umoja wa Mataifa na majukwaa mengine ya kimataifa.

Kwa upande wake, Mhe. Flemming Moller Mortensen amesema kwamba haikuwa rahisi kufikia uamuzi huo ambao umetokana na vipaumbele vipyta vya Serikali ya Denmark kwenye ushirikiano wa maendeleo kama ilivyoainishwa kwenye mkakati wake mpya uitwao "*The World We Share*".

Kwa mujibu wa Waziri Mortensen, mkakati huo mpya unaitaka nchi ya Denmark kufanya kazi kwa ukaribu zaidi na nchi zenye machafuko na migogoro (*fragility countries in conflict or crisis, displacement and irregular migration*) hususan katika

ukanda wa Sahel, Pembe ya Afrika na Nchi jirani za kanda hizo ambazo zina matatizo ya kisiasa.

Kadhalika, Waziri huyo amesema kwamba kutokana na Tanzania kufikia hatua nzuri ya maendeleo, Denmark imeamua sasa kufanya kazi kwa ukaribu na nchi tajwa ambazo ameeleza kwamba ndizo zenyetuhitaji zaidi na kwamba hatua hiyo haimaanishi uhusiano na urafiki kati ya Denmark na Tanzania unakufa au kufilia. Amemhakikishia Balozi Mulamula kuwa Denmark itaendelea kutekeleza makubaliano ya ufadhili (*financial commitments*) iliyokwishayafanya kwa Tanzania na itaendelea kuunga mkono jitihada za kuimarisha biashara, ukuaji wa uchumi, demokrasia na Sekta binafsi.

Mwisho, Waziri Mortensen ameeleza azma yake ya kufanya ziara nchini baadaye mwaka huu.

Imetolewa na:



Emmanuel Buhohela

Mkurugenzi, Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali.